*Toleo Maalumu*

# ITILIMA - DC

*Utekelezaji Miradi ya Maendeleo 2016/2020*

Toleo na. 01 | August 2020 | www. Itilimadc.go.tz

- **BILIONI 30 ZATEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO WILAYANI ITILIMA KWA MWAKA 2016-2020**
- **SEKTA YA MAJI PEKEE IKITUMIA BILIONI 14**




**Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Itilima ujenzi ukiwa umekamilika kwa awamu ya kwanza kwa thamani ya Tsh.Million 670.5, umejumuisha Mifumo ya Maji safi, Maji taka na Umeme na kuanza kutumika mapema mwaka 2018.**

# TAHARIRI

Mpenzi msomaji na Mfutiliaji wa Jarida la Itilima Dc lenye lengo la kuhabarisha Umma wa Tanzania kile kinacho tekelezwa na Ofisi Mkurugenzi mtendaji (W) hususani huduma zitolewazo kupitia Idara na Vitengo Mbalimbali vilivyopo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji halikadharika kuonyesha Miradi mbalimbali katika sekta ya Maji, Afya ,Elimu na Utawala iliyo tekelezwa katika kipindi hiki cha Serikali ya awamu ya 05 kwa mwaka wa fedha 2016-2020.

## DIRA/ (VISION)

*Kuwa na Taasisi yenye uchumi imara na shirikishi kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wote ifikapo 2022.*

## DHAMIRA/ (MISSION)

*Kutoa huduma bora na tosherevu kwa jamii kwa kutumia lasilimali zilizopo na kusimamia utawala bora kwa lengo la kuinua maisha ya watu.*

**Limeandaliwa na:**

**Kitengo cha Habari na Mahusiano kwa Umma**

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji**

**Halmashauri (W) Itilima**

**S.L.P 308**

**Bariadi, Simiyi**

Wilaya ya Itilima ni miongoni ya Wilaya 5 zinazounda Mkoa wa Simiyu, Ilianzishwa rasmi mwezi Machi mwaka 2012 kwa GN namba 73 na Halmashauri yake ilianzishwa Mwezi julai, 2013 kwa GN namba 47.

Wilaya ya Itilima ina eneo la Ukubwa wa Kilometa za Mraba 2,648 ambapo wastani wa kilometa za mraba 1,939

sawa na 73%, Zinatumika kwa Shughuri za Kiuchumi, Makazi na Miundombinu. kilometa za mraba 709 sawa na 27% ni maeneo ya vilima na hifadhi maalumu.

Wilaya imepakana na Wilaya ya Bariadi kwa upande wa Kaskazini; na upande wa Mashariki imepakana na Wilaya ya Ngorongoro Mkoa wa Arusha, Kusini imepakana na Wilaya ya Meatu na Kusini -Magharibi inapakana na Wilaya ya Maswa, na Upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Magu.

Maeneo ya Utawala, Wilaya ya Itilima ina Jimbo moja la uchaguzi, Tarafa nne, kata 22 , vijiji 102 na vitongoji 597 .

Eneo kubwa la Wilaya ya Itilima ni ardhi tambarare isiyo na milima mikubwa na ina mto mmoja mkubwa, mto Simiyu ambao hutiririsha maji yake kwenda katika ziwa Victoria.

Bonde la mto Simiyu katika wilaya ya Itilima ni kubwa kwa malinganisho na Wilaya nyingine zilizopitiwa.



**Waziri mkuuu Mhe. Kassim Majaliwa akikagua moja ya ghala la kuhifadhia pamba wilayani itilima**

Bonde hili limechukua eneo la Wastani wa Kilometa za Mraba zipatazo 69 sawa na wastani wa 3% ya eneo la wilaya.

Hata hivyo maji yake hutiririka katika misimu ya mvua tu, na si kwa mwaka mzima.

Hali ya hewa ya Itilima ni ya Joto kwa wastani wa 24°c-30°c. Wilaya ina vipindi viwili vya mvua ambayo ni vuli na

masika. Mvua za vuli huanza mwezi Oktoba na kuisha mwezi Desemba. Mvua za masika huanza Mwezi Machi na kuisha mwezi Mei.

Kipindi cha Januari hadi Februari mara nyingi huwa ni cha ukame, ambapo mara kadhaa mazao ya jamii ya nafaka huathirika kwa kiwango kikubwa.

Wastani wa Mvua ni kati ya milimita 700 – 900 kwa mwaka.

Eneo la upande wa Mashariki mwa Wilaya kuna sehemu kubwa ya Pori la Akiba la Wanyama la Maswa (Maswa Game Reserves) Pori hili lina ukubwa wa Kilometa za Mraba Zipatazo 640 sawa na Wastani wa 24% ya eneo la Wilaya. Poli hili linapakana na Hifadhi ya Wanyama ya Ngorongoro iliyopo Mkoani Arusha.

Idadi ya Watu kutokana na Taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, inaonyesha kuwa idadi ya watu katika wilaya Itilima ni 313,900, ambapo wanawake ni 165,398 na wanaume ni 148,502. Aidha, wilaya ina ongezeko la watu la wastani wa 1.8% kwa mwaka: kwa kuzingatia kiwango hicho,

idadi ya watu hadi kufika mwaka 2020 inakisiwa kuwa 348,779. Kaya moja ina wastani wa watu saba.

Shughuli kuu za kiuchumi za wakazi wa wilaya ya Itilima ni kilimo na ufugaji. Mazao ya chakula yanayo limwa ni mahindi, mtama, mpunga, muhogo, viazi vitamu na jamii ya mikunde. Mazao ya biashara ni pamoja na pamba, karanga na alizeti.

Aidha shughuli za ufugaji ni kubwa katika wilaya ikihusisha ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na bata.

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima inaundwa na Baraza la Madiwani wa Kuchaguliwa 22, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo lauchaguzi la Itilima, Waheshimiwa Wabunge wa Viti maaalumu na Madiwani wa Viti Maalumu na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Itilima.

# BILIONI 1.9 KUKAMILISHA JENGO LA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI ITILIMA

Halmashauri ya Wilaya ya itilima katika Mwaka wa fedha 2016/2017-2017/2018 ilipokea kiasi cha Tsh. Bilion Moja (1) kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, ambapo ujenzi huo utekelezaji ukiwa bado unaendelea kwa awamu ya II na ya III, baada ya awamu ya Kwanza kukamilika.

Awamu ya kwanza ya ujenzi ilikamilika April, 15.2018 na ulitekelezwa na Wakala wa Majengo ya Serikali – TBA, na ili gharimu kiasi cha Tsh. Milion 670.5 ambapo million 621.4 zilitumika kujenga miundombinu ya jengo yenye vyumba 43 na Mfumo wa maji safi na maji taka. Huku usimikaji wa mifumo ya umeme (Nguzo, transfoma na lines ukigharimu kiasi cha Tsh. Million 49.1 ambazo zililipwa Tanesco.

Awamu ya pili ya ujenzi unao tekelezwa kwa Mfumo wa FORCE ACCOUNT na kwa fedha zilizo baki katika awamu ya kwanza kiasi cha Tsh. Million 331.5, awamu hii mpaka kukamilika utagharimu kiasi cha Tsh. milion 481 na utakuwa na vyumba vya ofisi 28, Ukumbi 01, Kasiki 02, na mfumo wa maji safi, maji taka, mfumo wa umeme na mfumo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Hata hivyo Juni, 2020 Halmashauri ya Wilaya ilipokea kiasi cha Tshs. Milioni 900 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya tatu wa jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na ujenzi huo umeshaanza na upo katika hatua za awali za ukamilishaji Msingi wa jengo.Mradi huu ukikamilika utakuwa na vyumba 103, Ukumbi 01, Kasiki 02 na Maktaba 01.

Ujenzi wa ofisi hii umepunguza kwa asilimia 100(%) umepunguza msongamano uliyo kuwepo hapo awali kwa idara zote kukaa katika chumba kimoja , idara moja na nyingine zilitenganishwa na meza hali iliyo pelekea kutokuwepo kwa falagha katika kuwahudumia wateja waliyofika ofisini hapo kwa Mahitaji tofauti tofauti na mengine yenye kuhitaji falagha.



**Muonekano wa Jengo la ofisi ya mkurugenzi mtendaji baada ya awamu ya kwanza kukamilika, upande wa kulia ni muendelezo wa awamu ya pili ya ujenzi ukiwa katika hatua za umaliziaji.**



Jengo la awali lililokuwa likitumika kama ofisi ya Mkurugenzi mtendaji



**Aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Jumanne Sagini (katikati) akikagua jengo la ofisi ya Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri (W) itilima, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe. Benson Kilangi na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri (W) Itilima Bi. Elizabeth Gumbo**

# BILONI 14 ZABADILI HALI YA UPATIKANAJI WA MAJI SAFI NA SALAMA WILAYANI ITILIMA, KUTOKA 49% MWAKA 2015 HADI 64% 2020

Sekta ya maji kwa sasa wilayani itilima inendeshwa na Mamlaka ya usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mamlaka hii imeanzishwa kwa mujibu wa sharia Na. 5 ya usambazaji maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, ikiwa na jukumu la kupanga, kusanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa sasa wilayani Itilima ni asilimia 64 (%) ambapo mwaka 2015 hali ya upatikanaji wa huduma hiyo ilikuwa ni 49%

Wilaya ina jumla ya visima vifupi 1008 kati ya hivyo visima 734 vinafanya kazi kwa 100%, aidha wilaya ina malambo 21, mabwawa 3, visima virefu 42, Matanki 49 ya maji ya mvua katika taasisi na nyumba binafsi.

Aidha wilaya ina jumla ya miradi ya maji ya bomba 10, kati ya hiyo miradi saba inatoa huduma kwa wananchi, miradi hiyo ni ya Lagangabiili, Isengwa, Ikungulipu, Mwamapalala, Luguru, Inalo na Zanzui iliyojengwa kwa kutumia fedha ya miradi ya kitaifa (NWF).



**Vifaa vikia katika eneo la mradi kijiji Kabale**

Kwa sasa RUWASA inaendelea na utekelezaji wa upanuzi wa miradi sita kwenye vijiji vya Lagangabilili, Kabale, Zanzui, Mwamapalala, Ng'wang'ita na Ikungulipu iliyojengwa kwa kutumia feza za PBR, pia utekelezaji wa miradi ya P4R kwenye vijiji nane vya Laini A na B, Nguno, Shishani, Nyantugutu, Migato na Sawida na Mahembe na Gambasingu.



**Naibu waziri wa Maji Jumaa Aweso akitoa maelekezo ya ukamilishaji wa haraka wa mradi wa Maji Nkoma kwa viongozi wa itilima**

Usimamizi na Uendeshaji wa miradi hii utafanywa na Jumuhiya za watumiaji maji ngazi jamii (CBWSO) ambazo zimepewa jukumu hilo baada ya kusalijiwa na RUWASA kwa lengo la kutekeleza sharia Na. 5 ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 ambapo mpaka sasa RUWASA imesajili jumuhiya 18 katika vijiji 40 na kata 12 zoezi la usajili linaendelea katika kata 10 zilizo salia.

Fuatilia mchanganuo wa miradi yote ya maji wilayani Itililima ikiweo mipya na ukarabati iliyo tekelezwa katika kipindi hiki cha serikali ya awamuu ya tano inayo ongozwa Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli

Inaendelea Uk… 4 & 5

## MIRADI YA MAJI YA BOMBA

Miradi iliyo badilisha taswira ya hali ya upatikanaji maji wilayani Itilima ni miradi sita (06) mikubwa ya maji ya bomba, iliyo fanikiwa kupata kibali cha ujenzi katika kipindi cha mwaka 2016-2020 ni miradi katika Mji wa Lagangabilili,Isengwa, Ikungulipu, Mwamapalala,Kabale na Nkoma miradi hiyo ni kama inavyoonekana ktika jedwali lifuatalo

| Jina la Mradi | Gharama za mradi | Watu watakao nufaika na mradi hadi 2026 | Vituo vya kukingia maji (DP) |
|---|---|---|---|
| **Mradi wa Maji ya Bomba wa Mji wa lagangabilili** | **Mil. 907,951,739.66** | **4,268** | **21** |
| **Mradi wa maji ya bomba wa kijiji cha Kabale** | **Mil.150,381,622.50** | **4,860** | **13** |
| **Mradi wa maji ya bomba wa kijiji cha Isengwa** | **Mil. 560,675,621** | **4,407** | **16** |
| **Mradi wa maji ya bomba wa kijiji wa kijiji cha Mwamapalala** | **Mil. 237,580,326.03** | **6,179** | **15** |
| **Mradi wa maji ya bomba wa kijiji cha Ikungu-lipu** | **Mil. 242,176,875** | **14,794** | **13** |
| **Mradi wa maji ya bomba wa Nkoma** | **Bil. 1.3** | **6,961** | **22** |
| **Jumla** | **Bil. 4.5** | **41,469** | **100** |



**Mradi wa Matanki ya kusambazia Maji wa Ikungulipu**



**Mradi wa Maji ya bomba wa kijiji cha mwalushu**

## UJEZI WA MABWAWA MAKUBWA

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilipata kiasi cha Tsh. Bil. 3.25 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi wa Mabwawa manne (04) katika Kijiji cha Habiya, Sawida, Nhobora na Mwamapalala.

Mabwaha haya yanayotekelezwa na Wakala wa uchimbaji Visima na Utengenezaji wa Mabwawa (DDCA) itawanufaisha wakazi wapatao 27,598, Ng'ombe 11,141, Mbuzi 20,760 na Kondoo 6,895




**Muonekano wa Bwawa la Habiya baada ya kuka-**



**Muonekano wa Bwawa la Habiya kabwa ya ukarabati**



**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzana Mhe. Kassim Majaliwa akikagua Maendeleo ya Mradi wa Maji katika kata ya Nkoma**



**Wah. Madiwani pamoja na Wananchi wa Mwama-palala wakishiriki zoezi la upandaji wa Samaki katika bwawa la Mwamapalala**

## UCHIMBAJI NA UJENZI WA VISAMA

| Na. | Chanzo cha Fedha | Idadi ya Visima | Aina ya Visima | Gharama |
|---|---|---|---|---|
| 1 | DFID (PBR) | 19 | Vifupi | Mil. 72,045,000 |
| 2 | SERIKALI KUU | 40 | Virefu | Bil.1.6 |
| 3 | TASAF | 508 | Vifupi | Bil. 2.07 |
| Jumla | | 567 | | Bil. 3.6 |



Uchimbaji wa Kisi-
ma Kirefu katika
Kata ya Bumera



**Wananchi wa Kata ya Bumera wakipata Huduma ya maji baada ya kukamilika kwa mradi uchimbaji wa kisima kirefu**

## PICHA ZA MIRADI YA VISIMA VIREFU NA VIFUPI WILAYANI ITILIMA









## HOSPITALI YA WILAYA



**Jengo la wagonjwa wa nje la Hospitali ya wilaya ya Itilima**

Halmashauri Wilaya ya Itilima inaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zinazo lenga kuboresha utoaji wa huduma ya Afya kwa jamii ya wanaitilima.

Aidha wilaya inajumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 33 zikiwemo zahanati 29 na vituo vya Afya vitatu (03) na Hospitali moja ya Wilaya ikiwa ndiyo kwanza imeanza kutoa huduma ya Afya kwa wagonjwa wa nje kuanzia mwezi june,2020.

katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli Itilima ni miongoni mwa wilaya zilizo pokea kiasi cha Tsh. Bilioni 1.5 kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya wilaya na kufanikisha ujenzi wa majengo saba (7) ambayo ni jengo la Utawala, Jengo la Wagojwa wa nje (OPD), jengo la kufulia, jengo la wodi ya Wazazi, Jengo la Mionzi, jengo la Maabara na Jengo la kuhifadhia dawa.

Hata hivyo Serikali iliongeza kiasi cha Tshs. Milioni 300 kwa ajili ya ukamilishaji wa baadhi ya maeneo ya kipaumbele na kuanza kutoa huduma.

Kwa upande wa Vituo vya Afya na Zahanati, Wilaya ilipokea fedha kiasi cha Tshs. Bilioni 1.3 kutoka TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo katika Sekta ya afya kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2017/2018 ili kuboresha miundo mbinu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Vituo vya Afya vilivyo nufaika na fedha hizi ni Zagayu ambapo kuna mradi wa ujenzi wa Wodi ya Wazazi unaendelea wa Zaidi ya Tshs. Million 200, kwa ufadhili wa AMREF-Tanzania.

Kituo cha afya cha Nkoma Ujenzi wa jengo la huduma ya upasuaji wa dharura umekamilika kwa ufadhili wa Serikali ya Japan na Taasisi ya Benjamin Mkapa.

Kwa upande wa kituo cha Afya cha Ikindilo kilipata Zaidi ya Tshs. Milioni 500 kutoka Serikalini na UNFPA kwa ajili ya maboresho ya miundombinu, vifaa na ujenzi wa majengo mapya sita (06) ya Wodi ya Wazazi, Maabara, Jengo la Upasuaji, Jengo la kufuulia, jengo la kuhifadhia Maiti na Nyuma ya Mganga

Hata hivyo kupitia Mradi wa kuboresha Vituo vya kutolea Huduma za Afya kwa mpango wa malipo kwa Ufanisi (RBF), Wilaya ilipokea kiasi cha zaidi ya Tshs. Milioni 400.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma za afya na motisha kwa watumishi kwenye zahanati 29 na vituo 03 vya Afya

Hali ya upatikanaji wa dawa vituoni ni ya kuridhisha,hii ni kutokana na Serikali kuongeza bajeti ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka Tsh. Million 156.5 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Tsh. Milon 680 mwaka wa fedha 2018/2019. Katika fedha hizi Tsh. Million 475 ni fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu na Tshs. Million 209 ni kutoka mfuko wa pamoja wa Wahisani.






## ZAIDI YA MILIONI 500 ZIMEBORESHA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA AFYA CHA IKINDILO





Muonekano wa Njia za kupitia wateja na Watoa Huduma (walker way) za Kituo cha afya ikindilo



**Muonekano Mpya wa Kituo cha Afya Ikindilo Baada ya ujenzi kukamilika**



**Muonekano wa Chumba upasuaji katika kituo cha Afya Ikindilo**

## ELIMU MSINGI



Halmashauri ya wilaya ya Itilima ina jumla ya shule 91 za msingi zinazo milikiwa Serikali na kila shule ina darasa la Awali. Shule hizi zina julma ya wanafunzi 106,249 ni ongezeko la asilimia 35 (%) kutoka mwaka 2015 ambapo idadi ilikuwa Wanafunzi 78,688 na hii imechagizwa na uwepo wa mpango wa Elimu Bila Malipo.

Tangu kuanza kwa Mpango huu wa Elimu Bila Malipo kuanzia mwezi Desemba, 2015 hadi April, 2019 wilaya imepokea zaidi ya Tsh. Bilion 3.5. ikiwa ni Zaidi ya Tsh.bilion 2.2 kwa elimu Msingi na Zaidi ya Tsh. Billion 1.2 kwa elimu Sekondari.

Aidha mpango huu umekuwa wa Manufaa hususani kwa Wananchi wenye kipato cha chini kwani wameweza kupeleka watoto wao shule na kuongeza idadi ya wanafunzi wa darasa la awali kutoka 5,703 mwaka 215 ha kufikia Wanafunzi 16,018 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 117(%).

## SHULE YA MSINGI LALI



Idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza imeongezeka kutoka 6,203 mwaka 2015 hadi wanafunzi 16,018 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 158 (%).

Ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba umeongezeka kutoka 53% mwaka 2015 hadi kufikia 66.1 mwaka 2019

Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi

2017/2018 ilipokea fedha kiasi cha Tsh.milion 712.3 ambapo Milioni 145.2 zilizotolewa na EQUIP zilitumika kujengea madarasa sita (06) na ofisi tatu (03) matundu ya vyoo 21 na ujenzi wa Shule mpya za Italegunguhu, Ngando na Sali

vilevile kiasi cha Tsh. Million 707.3 kutoka P4R zilitumika katika ujenzi wa vyumba vya Madarasa 56, matundu ya vyoo 50 na ukarabati wa miundombinu ya shule

## SHULE YA MSINGI LAGANGABILILI









## ELIMU SEKONDARI

Kwa upande wa Elimu Sekondari, Wilaya ina jumla ya shule 30, ambapo shule 29 ni za Serikali na moja ni ya Taasisi ya Dini, zenye kidato cha kwanza hadi cha nne na shule mbili kati ya hizo ambazo ni Kanadi na Itilima Sekondali zina wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Shule hizi 29 zina jumla ya wanafunzi 7,970 kati yao wavulana ni 4,351 na Wasichana 3,619 na kwa shule moja binafsi ina jumla ya wanafunzi 283 kati yao wavulana 148 na wasichana 135, huku idadi ya walimu wa sekondari ikiwa 464 wanaume na 105 wanawake.

Katika uboreshaji wa miundombinu kwa shule za Sekondari, Wilaya ilipokea kiasi cha Tsh. Billion 1.15 kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 hadi 2017/2018 kutoka P4R kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 20, Mabweni matano (05), Maabara 10 na Matundu ya vyoo 44 na ukarabati wa miundombinu ya shule.

Aidha wilaya ilipokea kiasi cha Tsh. 178.4 kutoka Ubalozi wa China kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili (02) katika shule ya Sekondari Nkoma. Katika kipindi hicho hicho wilaya ilipokea fedha kiasi cha Tsh. Milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Mabwalo ya chakula katika Shule ya Sekondali Nkoma na Lagangabilili.

Hali ya ufaulu wa Mitihani ya kitaifa wilaya imekuwa ikifanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya kitaifa kwa kadato cha II, IV na VI kama inavyoonekana katika majedwali hapa chini

## UFAULU WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA II

| mwaka | Nafasi Kimkoa | Nafasi Kitaifa | % za Ufauli |
|---|---|---|---|
| 2016 | 1 | 4 | 98 |
| 2017 | 1 | 6 | 91 |

## UFAULU WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA IV

| Mwaka | Nafasi Kimkoa | Nafasi Kitaifa | % za Ufaulu |
|---|---|---|---|
| 2016 | 2 | 41 | 81.5 |
| 2017 | 2 | 30 | 87.2 |
| | | | |

## UFAULU WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA II

| Na. | Shule | Daraja (Division) | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | 0 | |
| 1. | Itilima | 2 | 26 | 36 | 1 | - | 65 |
| 2. | Kanadi | 2 | 22 | 14 | 2 | 1 | 41 |
| | **Jumla kuu** | 4 | 48 | 50 | 3 | 1 | 106 |

**SHULE YA SEKONDARI KANADI SEKONDARI KANADI**



**Mradi wa Madarasa ya P4R Shule ya Sekondari Kanadi**




MUONEKANA WA NDANI WA MADARASA **SHULE YA SEKONDARI KANADI SEKONDARI KANADI**



**Bweni la Wasichana katika Shule ya Sekondari Nkoma .**





**Naibu Waziri wa Elimu Mhe. Wilium Ole Nsha akizindua Bweni la Wasichana katika shule ya Sekondari Nkoma, Bweni hili lilijengwa kwa ufadhili wa Ubalozi wa China, kulia ni muonekano wa ndani wa Bweni hilo.**



**Naibu Waziri wa Elimu Mhe. Wilium Ole Nsha (katikati) akikagua Bweni la wasichana katika Shule ya ekondari Nkoma, Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Itilma Mhe. Benson Kilangi na Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Itilima.**

## MRADI WA MAABARA YA KISASA KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUDALABUJIGA SEKONDARI









Muonekano wa nje na ndani wa Maabara ya Kisasa ya Shule ya Sekondari Budalabujiga